

30



# KIBABII UNIVERSITY

## UNIVERSITY EXAMINATIONS

2021/2022 ACADEMIC YEAR

THIRD YEAR FIRST SEMESTER

### SPECIAL/SUPPLEMENTARY EXAMINATION

FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

COURSE CODE: SWA 313/KIS 308

COURSE TITLE: MBINU ZA UFUNDISHAJI

DATE: 14/11/2022

TIME: 11:00 AM - 1:00 PM

---

#### MAELEKEZO

Jibu maswali **matatu** pekee.

Swali la Kwanza ni la **lazima**.

MUDA: Masaa Mawili (2)

KIBU observes **ZERO** tolerance to examinations cheating

Maswali

- (a) Fasili dhana zifuatazo jinsi zinavyotumika katika elimu ya lugha. (alama 6)
    - i. Silabasi
    - ii. Nukuu za somo
    - iii. Stadi
  - (b) Tofautisha dhana ya ‘masuala ibuka’ na ‘udhibiti wa darasa’ katika muktadha wa elimu ya lugha. (alama 4)
  - (c) Mafunzo ya Kiswahili yanayotolewa kwa mwanafunzi kwa muda wa miaka minne yanatarajiwa kutekeleza madhumuni fulani ili kutimiza Malengo ya Elimu ya Kitaifa. Bainisha madhumuni hayo. (alama 8)
  - (d) Mbali na baadhi ya wasimamizi wa shule kulitweza somo la Kiswahili na kutukuza ya Kiingereza pamoja na sayansi, Kiswahili kinakabiliwa na ndaro anuai katika sekta ya elimu. Tetea hoja hii kwa kuzingatia hoja sita kisha utoe mapendekezo ya jinsi ya kuzikabili. (alama 12)
  2. Umeajiriwa kufunza Kiswahili kwa wanafunzi wasiozungumza Kiswahili kama lugha yao ya kwanza. Fafanua kanuni zozote utakazozingatia darasani unapofundisha lugha hii ukiegemea nadharia yoyote ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili. (alama 20)
  3. Mwalimu anayefundisha lugha ya pili anaweza kutumia njia moja au mseto wa njia kadhaa kuwafundisha wanafunzi wake. Pambanua nne kati ya njia hizo. (alama 20)
  4. (a) Ili kuainisha nyenzo, tunaweza kutumia vigezo viwili. Kigezo cha hisia zinazoathirika na kigezo cha uhalisia wa nyenzo zenyewe” (Kawoya, 1988). Onesha aina za nyenzo kwa kuzingatia vigezo hivyo viwili. (alama 10)  
(b) Fafanua madhumuni ya uandalizi wa ratiba ya somo. (alama 10)
  5. (a) Japo andao la somo na maazimio ya kazi ni nyenzo zinazoandaliwa na mwalimu na kuchukua nafasi ya dira katika somo la Kiswahili, nyenzo hizi zinatofautiana kwa vipengee kadhaa. Bainisha tofauti hizo. (alama 10)  
(b) Usetaji ndio mwelekeo wa kimaumbile katika ulimwengu wa sasa kwa mfano mavazi, mlo na kadhalika. Kwa kuzingatia ukweli huu, bainisha faida ya usetaji katika kufundisha Kiswahili. (alama 10)